

TOLEO LA. 09


Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKELAZA | APEWE TENA 5 | 8 SEPTEMBER, 2020



SENGEREMA, BUCHOSA WAMKUBALI MAGUFULI



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**



RAIS MAGUFULI: TUNAGHARAMIA WENYEWE UCHAGUZI MKUU

Na Mwandishi Wetu - **MWANZA**

Kwa mara ya kwanza, Tanzania imeweka historia ya kutumia fedha zake za ndani kiasi cha shilingi bilioni 330 kuendesha Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Kauli hiyo imetolewa na Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa mkutano wa hadhara wa kuomba kura ulifanyika leo mjini Sengerema mkoa wa Mwanza.

“Miaka mitano iliyopita wananchi wa wilaya hii mlituamini na ndio maana tumeweza kufanya haya makubwa ikiwemo uwezo wa kujitegemea na kufanya mambo makubwa kama kujenga daraja la Kigongo-Busisi litakalosaidia kukuza uchumi wa hapa na Taifa. Tuchagueni tena ili wasije wakaja watu wakaharibu mradi huu na hata kuuza vyuma vya ujenzi kama vyuma chakavu”, alisisitiza Rais Dkt. Magufuli.

Ametaja miradi itakayotekelezwa na kuwanufaisha wakazi wa Sengerema kuwa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Sengerema-Katunguru hadi Kamanga kwa kiwango cha lami ili kuondoa adha inayowakabili wananchi wanaotumia barabara hiyo na pia atatekeleza ahadi ya kuwajengea kwa kiwango cha lami barabara za Sengi, Nyampande, Nyantakubwa hadi Nyehunge.

Miradi mingine ni hospitali mbili zenye hadhi ya wilaya kwa gharama ya shilingi bilioni 3.8, miradi ya maji ya Sengerema kwa gharama ya shilingi bilioni 27.5, Vituo vya Afya vitano vya Kamanga, Nkome, Nyakaliro, Katunguru na Kagunga. Aidha, Serikali imeviko-pesha vyama vya ushirika mikopo sita na kujenga madara 167.



RAIS AANIKA MANUFAA MKATABA WA TANZANIA, KAMPUNI YA BARRICK

- Kulifanya Jiji la Mwanza Kitovu cha Biahara Afrika Mashariki

Na Mwandishi Wetu - **MWANZA**

Mkataba wa Serikali na kampuni ya uchimbaji madini ya Barrick nje ya fidia ya Dola milioni 300 na ongezeko la kodi na mrahaba, kampuni hiyo itatoa fedha nyingine zinazolenga kuchochea maendeleo ya mkoa Mwanza na maeneo yanayozunguka migodi hiyo na Taifa.

Hayo yamebainishwa na mgombea wa kiti cha Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli Jijini Mwanza katika Uwanja wa CCM Kirumba wakati wa mkutano wake wa kuomba kura kwa wakazi wa Jiji na mkoa huo.

“Chini ya Kifungu cha 8 cha Mkataba na nje ya makubaliano ya fidia Barrick wataipa Tanzania jumla ya Dola za Marekani zaidi ya milioni 100 sawa na shilingi bilioni 230, ambapo katika fedha hizo, dola milioni tano sawa na shilingi bilioni 11.5 zitatolewa kama mchango wa kutafiti kuhusu uwekezaji katika kuanzisha mradi wa kuchenjua madini yaani Smelter,” alisisitiza Rais Dkt. Magufuli.



Akifafanua zaidi Rais Magufuli amesema kuwa dola milioni 10 sawa na shilingi bilioni 23 zitatolewa kama mchango wa kuimarisha uwezo wa mitambo ya Serikali ya kupima viwango vya madini yanayozalishwa na hivyo kuimarisha uwezo wa kuku-sanya mrabaha.

Aliongeza kuwa dola milioni tano sawa na shilingi bilioni 11.5 zitatolewa kama mchango wa kuimarisha uwezo wa kuhifadhi madini katika migodi, wakati dola milioni 10 sawa na shilingi bilioni 23 zitatolewa katika kipindi cha miaka 10 kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuendeleza na kuimarisha mafunzo ya wataalamu wa madini na wahandisi wa uchimbaji madini na katika sayansi ya madini nchini.

Pia kwa mujibu wa mkataba huo, dola milioni 40 sawa na shilingi bilioni 92 zitatolewa ili zitumike kuboresha kiwango cha lami kutoka Jiji la Mwanza hadi mgodi wa Bulyanhulu pamoja na kujenga makazi ya wafanyakazi wa migodini katika Jiji hilo.

Aidha, kila mwaka dola sita katika kila ounce 1 ya dhahabu inayouzwa kupitia maki-nikia au dhahabu ghafi zitawekwa katika mfuko wa maendeleo kwa manufaa ya jamii zinazozunguka migodi. Hii ina maana katika wastani wa uzalishaji wa 'ounce' milioni 4.53 ni dola 27,180,000 sawa na shilingi bilioni 62.514 kila mwaka.

Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli anaendelea na mikutano ya kuomba ridhaa kwa wananchi kwa kipindi cha pili cha miaka mitano ili aweze kukamilisha ute-kelezaji wa miradi mikubwa na kusimamia vema rasilimali za nchi kwa maendeleo ya watanzania.



BUCHOSA YAPATA BARABARA YA LAMI KATIKA KAMPENI YA MAGUFULI

Na Mwandishi Wetu - Buchosa, **MWANZA**

Ni bahati ya 'Ngekewa' kwa wakazi wa Jimbo la Buchosa katika wilaya ya Sengerema mkoa wa Mwanza, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kutoa maelekezo ya kutangazwa zabuni ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya kilometa 42 kutoka Sengerema.

Rais Magufuli ametoa maelekezo hayo leo akiwa katikati ya kampeni jimboni Buchosa ambapo alitumia mamlaka yake kama Rais kumpigia simu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandishi Patrick Mfugale ili ahakikishe barabara hiyo inajengwa haraka.

"Upo wapi, sasa nakuagiza Mfugale kabla ya mwezi Desemba mwaka huu utangaze tenda ya kujengwa kwa barabara hii kwa kiwango cha lami na umjulishe na Waziri wa ujenzi, mimi si ndio Rais?," alitoa maelekezo na kusababisha wananchi kulipuka kwa furaha.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji Mkuu TANROADS, Mhandisi Patrick Mfugale alimhakikishia Mhe. Rais kwa njia ya simu kuwa watatekeleza agizo hilo.

Mgombea Urais kupitia chama cha Mapinduzi (CCM) Dkt. John Pombe Magufuli amekuwa ni Rais wa kipekee na mwenye mvuto ndani na nje ya Tanzania kutokana na uwezo wake wa kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua kwa haraka.



TUMCHAGUE DKT. MAGUFULI NI KIONGOZI MAKINI - MAJALIWA

Na Mwandishi Wetu - Hai, **KILIMANJARO**

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amesema watanzania wana kila sababu ya kumchagua Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, kwa sababu ni kiongozi makini, shupavu, mbunifu na mwenye uwezo wa kusimamia vizuri rasilimali za Taifa kwa manufaa ya wananchi wote.

Amesema katika kipindi cha miaka mitano ya awamu ya kwanza ya uongozi wake, Rais Dkt. Magufuli amefanya mambo mengi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini na yamewanufaisha Watanzania wote wakiwemo na wakazi wa wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Ameyasema hayo leo alipokuwa akimuomba kura Rais Dkt. Magufuli, mgombea Ubunge wa jimbo la Siha, Dkt. Godwin Mollel na wagombea udiwani kwa tiketi ya CCM kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika katika kijiji cha Matadi kata ya Ndemet wilaya ya Siha, Mkoani Kilimanjaro.

“WanaSiha wote nimekuja hapa kwenu leo nina kazi moja tu ya kumuomba kura mgombea wa nafasi ya urais kupitia CCM, Rais Dkt. Magufuli ambaye ni kiongozi imara, mzalendo na mchapakazi, mgombea ubunge wa jimbo la Siha Dkt. Mollel na wagombea udiwani wote wa CCM katika wilaya hii. Ikifika siku ya kupiga kura tuhakikishe tunawachagua.”

Kadhalika, Mheshimiwa Majaliwa ametumia fursa hiyo kuwahakikishia wananchi wa Siha kuwa Serikali itayarudisha mashamba yote ya Chama cha Ushirika cha Kilimanjaro (KNCU) yanayomilikiwa kinyemela na watu wachache kwa manufaa yao binafsi

“Kuna watu wamejamilikisha mahekari ya mashamba ya KNCU ambayo ni mali zenu, nawahakikishia tutawanyang’anya na kuyarudisha kwenu ili atakayelima alime, atakayefuga afuge”

Amesema KNCU ni mali ya wananchi (wanaushirika) na kwamba Serikali imefanya kazi kubwa ya kurudisha hadhi ya ushirika katika kipindi cha miaka mitano, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani waliohusika kufanya ubadhirifu katika vyama hivyo na itaendelea kurejesha mali zote kwa wananchi ili wafanyie shughuli za maendeleo.

Akizungumzia upatikanaji wa nishati ya umeme wilayani Siha, Mheshimiwa Majaliwa amesema kati ya vijiji 60 vilivyopo Siha vijiji vyenye umeme ni 58 na viwili tu ndio havina umeme na kwamba navyo vitaunganishwa umeme, amewaomba wakazi wake waendeleo kuwa na subira.

Amesema Rais Dkt. Magufuli anataka kuona kila nyumba ya Mtanzania inapata umeme tena kwa gharama nafuu na ametenga fedha nyingi zitakazotosheleza kusambaza umeme katika vijiji vyote kwa gharama za kuunganishiwa umeme huo ni shilingi 27,000 tu na kwamba wananchi hawatakiwi kulipia nguzo kwani Serikali imebeba gharama hizo.





JPM AWATAKA WANA-SENGEREMA KUTOKUUZA MAZAO HOVYO

• Aahidi Kujenga Maghala ya Kuhifadhi Mazao

Na Mwandishi Wetu - **SENGEREMA**

Mgombea wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli amewatahadharisha wananchi wa Wilaya ya Sengerema wasiuze mazao hovyo kabla ya msimu mwingine wa mavuno ili kuepuka kukumbwa na njaa.

Ametoa tahadhari hiyo leo Septemba 9, 2020 wilayani Sengerema mkoani Mwanza alipokuwa akiomba kura kwa wananchi hao ambapo aliwaambia kuwa ikiwa wataamua kuuza wauze ziada ya kile walichozalisha na bei iwe ya juu.

"Wakati wa ugonjwa wa COVID19 nchi nyingi ziliwafungia watu wake ndani hivyo hawakufanya kazi yoyote wana njaa, nchi inayotegemewa ni Tanzania kwa sababu sisi tuliendelea na shughuli zetu za kawaida hivyo tusiwe na tamaa ya kuyauza mazao yetu haraka haraka kwani tutapata njaa", amesema Rais Magufuli.

Katika kuhakikisha kuwa wilaya hiyo inakuwa na hifadhi ya kutosha ya chakula, Serikali imepanga kujenga maghala ya kuhifadhi chakula pamoja na kuanzisha masoko ya mazao.

Katika kampeni zake za Urais pamoja na kuwanadi wagombea Ubunge na Udiwani, Rais Magufuli amekuwa akipokelewa na umati wa watu kila anakopita na wengine maelfu wakijipanga barabarani kumpongeza kwa mabadiliko makubwa aliyoyafanya nchini kwa kipindi kifupi cha miaka mitano tu tangu aingie madarakani mwaka 2015.

Mpaka sasa Rais John Pombe Magufuli ameshafanya mikutano mikubwa katika Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mara na Mwanza. Rais Magufuli anatarajiwa kuen-
delea na mkutano wa kampeni kesho katika mkoa wa Geita kwenye Uwanja wa CCM Karangalala, Geita Mjini.



MAJALIWA: WANAHAI MSICHAGUE VIONGOZI KWA VIGEZO VYA UKABILA, UDINI

Na Mwandishi Wetu - Hai, **KILIMANJARO**

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa amewataka wakazi wa wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro wasichague viongozi kwa kutumia vigezo vya udini, ukabila, itikadi za vyama na badala yake wachague viongozi watakaokuwa tayari kushirikiana nao katika kuboresha maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Majaliwa ameyasema hayo leo wakati akimuomba kura Rais Dkt. John Pombe Magufuli, mgombea ubunge wa jimbo la Hai, Saasisha Mafuwe na wagombea udiwani kwa tiketi ya CCM kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika Kata ya Masama Kusini kwenye uwanja wa Kwa Sadala wilaya ya Hai, Mkoani Kilimanjaro.

“Ndugu zangu Watanzania, ndugu zangu wana-Hai na wana-Kilimanjaro mnatambua uwezo na uelewa mkubwa alionao Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli wa kutambua na kuona nini watanzania wanahitaji, nawaomba siku ya kupiga kura itakapofika tujitokeze kwa wingi bila kujali itikadi zetu tumpigie kura nyingi ili akaendeleze miradi ya maendeleo aliyoianzisha,” alieleza Majaliwa.

Amesema wakati umefika kwa wakazi wa Hai kuchagua kiongozi mwenye kujali na kutambua changamoto zinazowakabili katika maeneo yao na kushirikiana nao katika kuzitafutia ufumbuzi na kamwe wasikubali kupiga kura kwa ushabiki au kufuata mkumbo. Aliongeza: “Mchague Rais Dkt. Magufuli kwa nafasi ya urais na Saasisha nafasi ya ubunge pamoja na wagombea udiwani wote wa CCM.”

Mhe. Majaliwa amesema Rais Magufuli ni kiongozi anayetokana na Chama Cha Mapinduzi chenyewe utaratibu wa kuratibu miradi yote inayotakiwa kutekelezwa katika maeneo yote nchini kupitia ilani ya uchaguzi na kina mipango mizuri ya kuboresha maendeleo ya wananchi.

Wakati huo huo, Mheshimiwa Majaliwa amesema Serikali imedhamiria kumaliza tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika wilaya hiyo kupitia mradi mkubwa wa maji unaojengwa kwa sh. bilioni 520 kutoka Machame hadi Arusha. Visima vimekamiliwa kuchimbwa na usambazaji wa mabomba umeanza.

“Katika mradi huu wananchi wa Hai walio katika kilomita 12 kushoto na kulia kando kando ya maeneo ambayo bomba la maji litapita tutahakikisha Mamlaka ya maji AWSA inaweka matanki kwa ajili ya kusambaza maji kwa wananchi katika ukanda wa chini.”

Amesema shilingi bilioni 3.3 zimetumika kukamilisha mradi wa ujenzi na upanuzi wa skimu ya maji LOSAA - KIA. Maeneo yanayonufaika ni pamoja na kata ya Masama Magharibi, Masama Kati, Masama Kusini na kata ya KIA.

Mheshimiwa Majaliwa amesema sh. milioni 844 zimetumika kukamilisha ukarabati na ujenzi wa mifereji ya maji katika skimu za Nsanya, Musa Mwinjanga na Kikavu Chini. “Skimu ya Uroke - Bomang’ombe imekamiliwa na inahudumia maeneo ya Machame Uroki, Kwa Sadala, Kware, Romu na Mji wa Hai.



5 KALI ZA MAGUFULI WILAYANI SENGEREMA - MWANZA

01

Kuhusu maji hapa Sengerema tumetekeleza miradi ya maji yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 27.2 ikiwemo mradi mkubwa wa Nyamazugo - Sengerema uliogharimu shilingi bilioni 22, miradi mingine inaendelea hivyo tunaomba mtuamini tena miaka mitano mingine ili tukamilishe miradi hii ya maji.

02

Kuhusu miundombinu hapa Sengerema, tumekamilisha ujenzi wa gati la Ntama, tumejenga kiuuko cha MV Mwanza, tumeendelea na ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi. Tumejenga vyote hivyo kwa fedha zetu, hatujakopa kwa mtu yeyote kwa sababu Tanzania ni tajiri.

03

Katika kilimo hapa Sengerema tumepanga kujenga maghala ya kuhifadhi mazao na kuanzisha masoko ya mazao, Sengerema ni wakulima wazuri na ninawaomba msiyauze vibaya mazao yenu.

04

Nataka niwaahidi kuwa mkituchagua katika kipindi cha miaka mitano ijayo tutaijenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Sengerema - Katunguru hadi Kaman-ga yenye urefu wa jumla ya Kilomita 34.93.

05

Ni kwa mara ya kwanza Tanzania inafanya uchaguzi bila fedha za nje. Huko ndio kujitawala na kujitegemea, ninaomba tuendeleo kusimama imara tukijua tuko kwenye mikono salama ya Chama cha Mapinduzi ambayo inatupeleka mahali pazuri ambapo nchi inakwenda kujitegemea.



MOSHI WASEMA SASA IMETOSHA

• Waahidi Ushindi kwa Magufuli, Wabunge na Madiwani

Na Mwandishi Wetu - MOSHI

Utendaji kazi wa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais John Pombe Magufuli katika kuwaletea maendeleo wananchi Mkoa wa Kilimanjaro, umewafanya wakazi wa wilaya hiyo kujenga Imani kubwa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) na kukiweka Chama hicho katika nafasi ya kupata kura za kishindo katika majimbo ya Moshi Mjini na Moshi Vijijini.

Wakiongea katika mahojiano maalum katika maeneo tofauti Mjini Moshi, kuhusu uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu, wamesema kuwa sasa ni wakati muafaka kwa CCM kuongoza majimbo yote ya Mkoa wa Kilimanjaro kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano.

"Hii Serikali ya Magufuli haitaki mzaha, inachapa kazi tu mpaka sisi vijana wa hapa Moshi tumeona treni ambayo itarahisisha usafirishaji wa bidhaa. Haya mambo

hatujawahi kuyaona tangu tuzaliwe zaidi ya kuona reli tu," anaeleza Honest Rogasian wa Majengo.

"Kuna vijana huku kaskazini toka wamezaliwa mpaka wamefikia umri wa kupiga kura hawakuwahi kuona treni ikipita juu ya reli, lakini kwa miaka mitano wameona," anaeleza Mzee Joseph Muro wa Kitandu kati, Kibosho, Wilaya ya Moshi vijijini huku akisisitiza kumnadi Rais Magufuli ashinde kwa kishindo.

Emmanuel Masawe mkazi wa kata ya Kibosho Kirima wilaya ya Moshi vijijini, ambaye ni mhitimu wa shahada ya kwanza ya uchumi Chuo Kikuu cha Dar es salaam anasema ujenzi wa miundo mbinu inayokidhi mahitaji ya kisasa ndio msingi mkuu wa kuinua uchumi wa Tanzania na Rais Magufuli ameonesha njia na anastahili kulitumikia Taifa kwa awamu ya pili kwa kuwa tunaimani naye.



BILIONI 12 KUPELEKA NEEMA YA MAJI MISUNGWI

Na Mwandishi Wetu - Misungwi, **MWANZA**

Wakazi wa Shilingi bilioni 12 kuleta neema ya maji kwa wakazi elfu 64 wa wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza ikiwa ni moja ya hatua za kukuza ustawi wa wananchi.

Hayo yamesemwa na Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa mkutano wake katika eneo la Usagara wilaya ya Misungwi, akiwa njiani kuelekea mkoani Geita ambako atakuwa na mkutano mkubwa wa hadhara.

Mbali na maji, Mhe. Rais amesema kuwa Serikali yake imetumia shilingi bilioni 6.6 kutoa elimu bila malipo ili kukuza elimu, na kutoa fursa kwa watoto wote hasa wa wanyonge kupata elimu bure. Tumejenga madarasa, maabara na kufanya upanuzi wa

hospitali ya wilaya ya Misungwi na kuimari-sha huduma za jamii,” amesisitiza Rais Magufuli.

Kwa upande wake Bw. Alexander Mnyeti ambaye ametipa bila kupingwa katika jimbo la Misungwi, amesema kuwa wananchi wa jimbo hilo watampa kura zote Rais Dkt. Magufuli na ingekuwa uamuzi wao wangemruhusu mgombea huyo akapumzike asubiri kupata ushindi wa kishindo kutokana na wingi wa kura atakazopigiwa na watanzania.

Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi Dkt. John Pombe Magufuli ameagwa na wananchi wa mkoa wa Mwanza ambao walijitokeza kwa wingi kumshangilia wakati msafara wake ukielekea Sengere ma na baadae mkoani Geita.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**